# DISTINCTION SCHOOL BASED ASSESSMENT TEST

# DARASA LA NANE - 2023

## UTABIRI THABITI

## KISWAHILI: LUGHA

EDUCATIONAL PUBLISHERS DISTINCTION 002 QUALITY IS OUR CONCERN 002

8 PREMIER

*Muda: Saa 1 dak 40*

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.**

Kufaulu kwa Maridhia katika masomo ____1_____ wakazi wengi wa kaunti _____2____ Kakamega. Kijana huyo alipitia changamoto nyingi mno. _______3______, aliendelea kujikaza bila _____4_____. Alipokosa karo ya ______5____ masomo yake ya chuo kikuu, aliajiriwa kuwa yaya. Kwa njia hiyo, ______6_____ akiba katika benki bila kuchoka. Alielekezwa na msemo kuwa _______7______. Alipokusanya kiasi cha kutosha, alianza kuhudhuria vipindi kila ______8_____ jua lilipoelekea kutua. Hivyo ndivyo alivyomudu kuwa daktari wa watoto. Wengi humwangalia kama mfano bora katika jamii.

1. A. kuliwashangaza B. aliwashangaza C. yaliwashangaza D. waliwashangaza
2. A. za B. la C. cha D. ya
3. A. Lakini B. Aidha C. Ingawa D. Hata hivyo
4. A. kufanya juhudi B. kufua dafu C. kupiga moyo konde D. kufa moyo
5. A. kugharimu B. kugharamia C. kugharimia D. kugharama
6. A. aliwekeza B. aliweka C. aliwekesha D. aliwekewa
7. A. bandu bandu huisha gogo B. kinga na kinga ndipo moto uwakapo C. chururu si ndondondo D. haba na haba hujaza kibaba
8. A. machweo B. alasiri C. adhuhuri D. macheo

Watoto wanafaa kuonywa _____9_____ ubadhirifu ______10______ wanapokuwa wachanga. Ubadhirifu ni tabia ya ______11_____ vitu kama vile chakula, pesa, sabuni, maji na kadhalika. Wanafaa ______12_____ kuwa ni vyema kutunza kile walicho nacho na _____13_____ kwa uangalifu. Kwa kuelewa kuwa watoto ______14_____ ndio viongozi wa kesho, tutakuwa tukihakikisha kuwa watakuwa viongozi bora na waadilifu. _______15____ rasilimali za nchi vibaya.

9. A. kati ya B. minghairi ya C. licha ya D. dhidi ya
10. A. hadi B. tangu C. vile D. jinsi
11. A. kuvuja B. kufuja C. kuvunja D. kuhifadhi
12. A. kusisitiza B. kusisitizwa C. kusisitiziwa D. kusisitizia
13. A. kuitumia B. kukitumia C. kujitumia D. kuutumia
14. A. hawo wao B. hao wao C. wao hawo D. wao hao
15. A. Hawatatumia B. Watatumia C. Hatutatumia D. Tutatumia

**Kuanzia nambari 16 hadi 30 jibu kulingana na maagizo.**

16. Tambua wingi wa;
***Mama amepika mkunga akala.***
A. Wamama wamepika mikunga wakala.
B. Akina mama wamepika wakunga wakala.
C. Akina mama wamepika mikunga wakala.
D. Wamama wamepika wakunga wakala.

17. Msimu wa baridi kali bila mvua huitwaje?
A. masika B. kiangazi
C. kipupwe D. mawaga

18. Chagua ukanusho wa sentensi ifuatayo.
***Ningekamilisha kazi ningepumzika.***
A. Nisingekamilisha kazi nisingalipumzika.
B. Singekamilisha kazi singepumzika.
C. Nisingekamilisha kazi nisingepumzika.
D. Nisingalikamilisha kazi nisingepumzika.

19. Tambua matumizi ya '**ki**' kwenye sentensi ifuayo.
***Akitembea vibaya ataanguka kitoto.***
A. masharti, udogo
B. msharti, namna
C. wakati, jinsi
D. wakati, udogo

20. Ruka ni kwa <u>rukia</u> kama vile weka ni kwa____.
A. wekwa B. wekea
C. wekeka D. wekeana

21. Sentensi gani iliyotumia ritifaa?
A. Alizuru miji mingi: Nakuru, Mombasa, Mumias, Naivasha na Nairobi.
B. Mbu, utitiri, chawa na mbung'o ndio vimelea anaowajua.
C. Wakazi wengi wamehuzunika; hali ya maisha imekuwa ngumu.
D. Nimeelewa vyema kuwa asiyesikia la mkuu...

22. Ikiwa juzi ilikuwa 'Jumatano', mtondo itakuwa;
A. Jumapili B. Jumamosi
C. Jumanne D. Jumatatu

23. Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mistari.
Ala! Kwa nini umeingia ndani ya nyumba chafu?
A. kiunganishi, kihusishi
B. kihusishi, kihisishi
C. kihisishi, kihusishi
D. kihisishi, kiunganishi

24. Kivumishi gani kinachoweza kuundwa kutokana na kitenzi '**cheka**'?
A. kicheko B. ucheshi
C. mcheshi D. chekesha

25. Umati ni wa watu, koja ni la ________.
A. funguo B. mboga
C. maua D. nyuki

26. Sentensi gani iliyo sahihi kati ya sentensi zifuatazo?
A. Atayewasili mapema ataingia bila malipo.
B. Kiti ambacho kilichovunjika ni chake.
C. Wageni wakujao hapa ni wa mjomba.
D. Anywaye maji mengi huimarisha afya.

27. Kiambishi '**po**' kimetumikaje kwenye sentensi ifuatayo?
***Walipowasili walipigiwa makofi.***
A. kuonyesha wakati
B. kuonyesha namna
C. kuonyesha mahali
D. kuonyesha masharti

28. Mshororo ufuatao una mizani mingapi?
Ewe mwanangu jikaze, kweli usilaze damu,
A. 2 B. 16
C. 8 D. 17

29. Chagua nomino inayopatikana katika ngeli tofauti na zingine?
A. manukato B. mazingira
C. maradhi D. maovu

30. Tambua jibu linaloonyesha sudusi mbili.
A. $\frac{2}{6}$ B. $\frac{6}{2}$
C. $\frac{2}{5}$ D. $\frac{2}{7}$

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Ukame una madhara chungu nzima kwa binadamu. Madhara hayo huweza kuwa ya kiuchumi, kimazingira au hata kijamii. Ukame husababisha kupungua kwa mimea na mavuno. Huweza pia kutokea dhoruba za mchanga. Dhoruba hizi hutokea palipo na jangwa. Ukosefu wa maji ya kunyunyizia mimea husababisha njaa na magonjwa kama vile utapiamlo yanayotokana na ukosefu wa lishe bora.

Makazi ya wanyama wa nchi kavu na wale wa majini pia huathiriwa vibaya. Halikadhalika, ukame husababisha uhamaji. Hii inamaanisha kuwa jamii huweza kutoka katika makazi asilia na wakati mwingine huweza hata kuwa wakimbizi.

Ukame husababisha ukosefu mkubwa wa maji. Ukosefu huu huwa na athari hasi kwa maendeleo ya viwanda kwa kuwa vingi huhitaji kiasi kikubwa cha maji. Juu ya hayo, maji huhitajika katika kuzalisha umeme. Umeme una matumizi mengi katika viwanda, nyumbani, afisini na hata hospitalini. Ukosefu wa umeme basi huwa ni tatizo kuu.

Aidha, ukame unajulikana kusababisha uhasama wa kijamii. Jamii huweza kuzozana na hata kupigana kutokana na uhaba wa rasilimali za asili kama vile chakula na maji. Hali kama hiyo huwafanya watu waishi katika hali ya kuteseka. Pia mioto mikubwa huweza kuenea haraka wakati wa ukame na hivyo kusababisha vifo vya binadamu na wanyama na uharibifu wa rasilimali nyingine.

Ingawa ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana nao kwa kupunguza makali ya ukame. Jambo la kwanza wanaloweza kufanya binadamu ni kuhifadhi maji. Maji ya mvua yanafaa kuhifadhiwa katika mabwawa na mapipa.

Haya yanaweza kutumiwa wakati wa ukame hasa katika kukuza mimea. Mkakati mwingine ni kutumia mbinu za kupunguza chumvi na kemikali nyingine zilizomo kwenye maji ya bahari ili yaweze kutumika katika unyunyiziaji wa mimea. Hili litapunguza tatizo la ukosefu wa chakula.

Pia ni muhimu kufanya utafiti kuhusu hali ya anga ili kupanga na kuweka mikakati ifaayo kukabiliana na hali hiyo.Ni muhimu kuwa na mipangilio mizuri ya matumizi ya ardhi. Mathalani upanzi wa mimea itakayozuia mmomonyoko wa udongo, kubadili aina ya mimea inayokuzwa sehemu fulani pamoja na upanzi wa mimea isiyohitají mvua nyingi katika maeneo kame ni hatua mwafaka. Aidha, ni vizuri kupunguza matumizi ya maji hasa katika mazingira ya nyumbani kwa mfano tunapofua na kuosha. Njia nyingine ya kukabiliana na tatizo hili ni kusafisha maji yaliyotumiwa ili kuyatumia tena.

31. Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa;
A. Ukame huleta madhara chungu nzima kwa binadamu.
B. Ukame husababisha kukauka kwa mimea na mavuno.
C. Ukame husababisha kutokea dhoruba za mchanga kila mahali.
D. Ukame huweza kusababisha ukosefu wa lishe bora.

32. Mwandishi anasema kuwa ukame huweza kudhuru yafuatayo ila;
A. jamaa
B. uchumi
C. mazingira
D. jamii

33. Badala ya kutumia neno '**kuteseka**' mwandishi angetumia nahau gani?
A. kula mwata
B. kula mumbi
C. kula muku
D. kula mlungula

34. Ni kweli kuwa ukame una madhara kwa;
A. nchi kavu na majini.
B. maendeleo kwa jumla.
C. ukuaji wa viwanda.
D. uhamaji kutoka mahali

35. Kwa mujibu wa kifungu, viwanda vinahitaji nini ili kufanya kazi?
A. maji na umeme
B. wafanyakazi na umeme
C. maji na upepo
D. upepo na wafanyakazi

36. Kulingana na aya ya nne, ni kweli kuwa;
A. Uhasama wa kijamii unaosababishwa na ukame unajulikana.
B. Jamii zimekuwa zikizozana na kupigana kutokana na uhaba wa chakula na maji.
C. Ukame ndiyo sababu kuu ya kutokea kwa mioto mikubwa katika misitu.
D. Uhasama wa kijamii unaweza ukazuiwa au kupungua ikiwa ukame utazuiwa.

37. Aya ya nne inaweza ikarejelewa kwa methali gani?
A. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo.
B. Aisifuye mvua imemnyea.
C. Usipoziba ufa utajenga ukuta.
D. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

38. Kupunguza chumvi na kemikali nyingine zilizomo kwenye maji ya bahari kuna faida gani?
A. Hupunguza ukame katika jamii.
B. Hupunguza tatizo la uhaba wa chakula.
C. Humaliza tatizo la ukosefu wa chakula.
D. Huhakikisha kuwa kuna maji safi na salama ya kunywa.

39. Gani si kati ya mikakati ya kukabiliana na hali ya ukame kulingana na aya ya mwisho?
A. kupanda mimea inayozuia mmomonyoko wa udongo
B. kupanda mimea inayosababisha mvua nyingi kunyesha
C. kubadili aina ya mimea inayokuzwa sehemu fulani
D. kupanda mimea isiyohitají mvua nyingi

40. Chagua kichwa kinachofaa kwa makala haya.
A. Madhara ya ukame
B. Jinsi ya kuzuia ukame
C. Athari na uzuiaji wa ukame
D. Jinsi ya kuishi katika sehemu kame

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.</u>***

Kisa cha Mfalme Mazurui husimuliwa na jamii nyingi kwa msisimko mkubwa. Wapo wanaopenda kukisikiliza wakila huku wengine wakisikiliza wakiota moto. Wajukuu wengi hupenda kuwasumbua akina nyanya na babu zao wawasimulie kisa hicho tena na tena. Yaani, huwa kama chakula ambacho hata leo ukila na kushiba vipi, bado utatamani kingine kesho. Mimi nimewahi kusimuliwa na nyanya yangu kama mara kumi na mbili hivi. Aidha, siwezi nikahesabu ni mara ngapi babu amesimulia kisa kicho hicho.

Mfalme Mazurui alijulikana kote pote na mote kwa utajiri wake. Hakika, **alijulikana kama pesa**. Kila wakati alipenda kwenda kuwinda wanyama wa porini pamoja na mfanyakazi wake aliyempenda sana. Mfanyakazi huyo naye alipenda kusema, "Kila jambo linalotufanyikia, Mungu huliruhusu akiwa na sababu. Huwa anataka kutusaidia." Siku moja walipokuwa wakiwinda, Mfalme alikamatwa na mnyama hatari na kuangushwa chini. Baada ya kusumbuana kwa dakika karibu kumi, Mfalme alifaulu kujiokoa lakini kidole chake kimoja cha mkono kilikuwa kimekatika. Mfanyakazi wake alimwambia, "Shukuru Mungu, ameruhusu ukatike kidole. Hapo anataka kukusaidia." Mfalme alikasirika sana na kumtupa mfanyakazi wake jela.

Siku kadhaa baada ya kupona, Mfalme **alikata shauri** kwenda kuwinda akiwa pekee yake. Kwa bahati mbaya, alipatikana na majambazi waliokuwa wakiua watu kama sadaka kwa miungu yao. Mfalme alipigwa na butwaa karibu aanze kulia. Alijaribu kuwaomba wasimwue lakini walikataa katakata. Walimfunga mikono na miguu. Baadaye walimweka kwenye kuni zilizokuwa

zimekauka. Walipokaribia kumchinja waligundua kuwa mfalme hakuwa na kidole kimoja. Walikasirishwa sana kwa sababu hawakufaa kumchinja mtu asiye na sehemu yoyote ya mwili. Mfalme alifunguliwa na kuruhusiwa kuelekea nyumbani.

Mfalme sasa aliona umuhimu wa kukosa kidole kimoja. Kumbe angekuwa na vidole vyote angechinjwa na majambazi hao. Alipofika nyumbani, aliamrisha mfanyakazi yule afunguliwe. Alipoachiliwa, Mfalme aliomba msamaha na kusema, "Kweli nimeamini kwamba Mungu aliruhusu nikatike kidole ili nisaidike. Leo nisingekuwa hai kama ningekuwa na vidole vyote." Mfanyakazi wake hakusema chochote. Alinyamaza tu.

Baadaye mfalme alimwuliza mfanyakazi swali, "Kuna jambo ambalo sijaelewa. Kwa nini Mungu aliruhusu nikufunge jela ilhali hukuwa na makosa?" Mfanyakazi alicheka kidogo kisha akamjibu, "Mfalme, ulinifunga kwa kuwa ningeenda na wewe, majambazi hao wangeniua kwa sababu mimi nina vidole vyote." Mfalme aliandaa sherehe kubwa ya kumshukuru Mungu kwa ulinzi wake. Aidha, aliwakumbusha wakazi wa eneo lote kuwa kila mtu ana sababu ya kumshukuru Mungu. Asiyekuwa na viatu amshukuru Mungu kwa kuwa ana miguu. Asiyekuwa na miguu amshukuru Mungu kwa kumpa uhai.

**41.** Aya ya kwanza inaeleza kuwa;
A. Kisa cha Mfalme Mazurui husimuliwa na jamii kwa msisimko mkubwa.
B. Msimulizi amewahi kusimuliwa kisa cha mfalme Mazurui zaidi ya mara kumi na mbili.
C. Msimulizi hupenda kuwasumbua nyanya na babu yake wamsimulie kisa cha mfalme Mazurui tena na tena.
D. Msimulizi anapokula chakula na kushiba vipi bado hutamani kingine keshoye.

**42.** Maneno **'alijulikana kama pesa'** ni mfano wa tamathali gani ya lugha?
A. tanakali
B. sitiari
C. tashbihi
D. nahau

**43.** Yawezekana kuwa Mfalme Mazurui alisumbuana na mnyama kwa muda wa;
A. dakika kumi
B. dakika tisa
C. dakika tatu
D. dakika kumi na moja

**44.** Maneno **'alikata shauri'** yana maana gani jinsi yaivyotumika katika kifungu?
A. alishauriwa
B. aliamua
C. alilazimika
D. alidanganyika

**45.** Ni kweli kuwa mfalme alipokutana na majambazi;
A. alianza kulia kutokana na kupigwa.
B. aliwekwa kwenye kuni zilizokuwa zimekauka na kuchinjwa.
C. alikaribia kulia kutokana na mshangao aliokuwa nao.
D. alikasirika alipogundua kuwa hakuwa na kidole kimoja.

**46.** Kufungwa jela kwa mfanyakazi wa mfalme kulikuwa na manufaa gani?
A. Kulifanya mfalme asiuawe na majambazi
B. Kulimwepushia mfanyakazi kuuawa na mnyama
C. Kulimwepushia mfanyakazi kuuawa na majambazi
D. Kulifanya mfalme asiuawe na mnyama hatari.

**47.** Kulingana na aya ya mwisho, mfalme hakuelewa;
A. sababu ya Mungu kuruhusu akatike kidole.
B. kosa lililofanya amfunge mfanyakazi wake.
C. kwa nini majambazi hawakumwua.
D. sababu ya Mungu kuruhusu amfunge mfanyakazi wake bila kosa.

**48.** Yaonekana kuwa mfalme katika kifungu hiki alikuwa na sifa gani?
A. katili na mjinga
B. mjanja na mwaminifu
C. katili na mnyenyekevu
D. karimu na mwenye bidii

**49.** Chagua mpangilio unaofaa wa matukio katika kifungu hiki.
A. kuandaa sherehe, kukatika kidole, kupatikana na majambazi
B. kupatikana na majambazi, kukatika kidole, kutiwa mbaroni
C. kukatika kidole, kutiwa mbaroni, kupatikana na majambazi
D. kushambuliwa na mnyama, kufungwa jela, kukatika kidole

**50.** Funzo kuu linalotokana na kisa hiki ni kuwa;
A. tumshukuru Mungu katika kila jambo.
B. tumshukuru Mungu mara nyingi.
C. tusiwawinde wanyama wa porini.
D. tumshukuru Mungu kila mahali.